



CHUO KIKUU CHA TAIFA CHA ZANZIBAR (SUZA)
TANGAZO KWA WAOMBAJI WALIOCHAGULIWA AWAMU YA
KWANZA KATIKA MWAKA WA MASOMO 2023/2024

UTANGULIZI

Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) kinapenda kuutaarifu umma kuwa kimetoa orodha ya wanafunzi waliochaguliwa kujiunga na masomo awamu ya kwanza kwa ngazi ya Cheti, Diploma na Digrii kwa mwaka wa masomo 2023/2024 kwa program mbalimbali kama zinavyojionesha katika kiambatanisho hapo chini.

BARUA YA UDAHILI NA VIAMBATANISHO VYENGINE

SUZA inawaomba waombaji wote waliochaguliwa wahakikishe wanaingia katika akaunti zao walizotumia wakati wa kuomba chuo (baruapepe/*email* na *password* iliyotumika wakati wa kuomba) kwa lengo la kupata barua za udahili (**Admission letter**) pamoja na viambatanisho vyengine muhimu vya kujiunga na chuo.

WALIODAHILIWA CHUO ZAIDI YA KIMOJA (MULTIPLE SELECTION)

Kwa waombaji wa shahada ya kwanza (Degree) ambao wamechaguliwa chuo zaidi ya kimoja (**multiple selection**), wanashauriwa kuingia katika akaunti zao na kuthibitisha (**confirmation**) kwa kutumia nambari ya siri (**confirmation code**) ambayo wamerushiwa na Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU) kupitia nambari zao za simu au barua pepe walizotumia

wakati wakiomba chuo. Kama bado hujatumiwa nambari ya siri, ingia kwenye akaunti na uiombe kupitia sehemu iliyoandikwa **request confirmation code**. Uthibitisho huo (**confirmation**) unatakiwa ufanywe baina ya tarehe **28 Agosti**, hadi tarehe **6 Septemba, 2023**.

KUFUNGULIWA KWA DIRISHA LA PILI LA MAOMBI

Chuo kinawataarifu wale wote ambao ***hawakufanikiwa kuchaguliwa*** kwa awamu ya kwanza, waombe kozi nyengine ambazo wana sifa nazo zilizotangazwa na chuo kwa awamu ya pili itakayoanza tarehe **28/08/2023** hadi **03/09/2023**. Kozi zinazotolewa awamu ya pili zimeambatanishwa katika tangazo hili.

HITIMISHO

SUZA inawaomba waombaji wote wasisite kuwasiliana na maafisa udahili katika kampasi tafauti za chuo kwa msaada zaidi.

Tangazo hili limetolewa na:

Kurugenzi ya Shahada za Awali (DUS)

Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar